## Siku ya Uamsho wa Mabadiliko ya Majira
## Day of Action on Climate Change

**Dec. 8. 2007**

Tanzania Coalition for Sustainable Development (TCSD) kwa kushirikiana na Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA) tunashirikiana kuandaa msafara wa baisikeli hapa Dar es Salaam kwa ajili ya Siku ya Uamsho wa Mabadiliko ya Majira jumamosi tarehe 8 Disemba. Kwenye siku hiyo mashirika mengi duniani yanaandaa matukio mbali mbali – kwa taarifa zaidi tembelea tovuti hii www.globalclimatecampaign.org . Mwezi huu serekali za dunia zinakutana jiji la Bali, Indonesia kufanya uamuzi kuhusu mabadiliko ya majira.

Mabadiliko ya majira duniani yanasababishwa na moshi wa carbon dioxide unaotolewa wakati fossil fuels zinachomekwa. Maana ya fossil fuels ni mafuta na gesi kutoka chini ya ardhi. Zinaunguzwa kwenye magari, viwandani na kuzalishia umeme. Carbon dioxide inaenda juu sana na haina mpaka – carbon dioxide inayozalishwa kwenye nchi moja ina matokeo mabaya kwa majira ya nchi zote. Carbon dioxide hiyo inakuwa kama blanketi juu ya dunia na kusababisha majira yawe ya joto zaidi, kubadalisha mfumo wa mvua na kuongeza kiwango cha maji baharini. Hali ya mabadiliko haya imeanza kujitokeza hapa Tanzania. Mfano wakulima hawapati mvua kwa wakati kama zamani na kiwango cha mvua kimepungua katika maeneo mengi.

Ili kurekebisha tatizo la mabadiliko ya majira ni lazima kutumia teknolojia mbadala mbali na fossil fuels. Mfano tunaweza kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya mto, nguvu za jua na upepo. Tunaweza kutengeneza mafuta ya magari kwa kutumia mafuta ya mazao (biofuel). Pia, tunaweza kupata gesi safi kutoka mbolea (biogas). Tunaweza kupanda miti ambayo huchukua carbon dioxide kutoka kwenye hewa wakati inakua. Carbon dioxide hiyo hutoka tena na kurudi hewani wakati miti hiyo inapounguzwa lakini kwa ujumla carbon dioxide haiongezeki (biomass).

Wachangiaji wakubwa wa shida hii ya mabadiliko ya majira ni nchi tajiri, kwa sababu wao wanatoa kiasi kikubwa sana cha carbon dioxide. Basi wana wajibu wa kupunguza kiasi cha carbon dioxide wanayozalisha na pia kusaidia nchi masikini kutumia technolojia mbadala.


## Siku ya Uamsho wa Mabadiliko ya Majira
## Day of Action on Climate Change

**Dec. 8. 2007**

Tanzania Coalition for Sustainable Development (TCSD) kwa kushirikiana na Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA) tunashirikiana kuandaa msafara wa baisikeli hapa Dar es Salaam kwa ajili ya Siku ya Uamsho wa Mabadiliko ya Majira jumamosi tarehe 8 Disemba. Kwenye siku hiyo mashirika mengi duniani yanaandaa matukio mbali mbali – kwa taarifa zaidi tembelea tovuti hii www.globalclimatecampaign.org . Mwezi huu serekali za dunia zinakutana jiji la Bali, Indonesia kufanya uamuzi kuhusu mabadiliko ya majira.

Mabadiliko ya majira duniani yanasababishwa na moshi wa carbon dioxide unaotolewa wakati fossil fuels zinachomekwa. Maana ya fossil fuels ni mafuta na gesi kutoka chini ya ardhi. Zinaunguzwa kwenye magari, viwandani na kuzalishia umeme. Carbon dioxide inaenda juu sana na haina mpaka – carbon dioxide inayozalishwa kwenye nchi moja ina matokeo mabaya kwa majira ya nchi zote. Carbon dioxide hiyo inakuwa kama blanketi juu ya dunia na kusababisha majira yawe ya joto zaidi, kubadalisha mfumo wa mvua na kuongeza kiwango cha maji baharini. Hali ya mabadiliko haya imeanza kujitokeza hapa Tanzania. Mfano wakulima hawapati mvua kwa wakati kama zamani na kiwango cha mvua kimepungua katika maeneo mengi.

Ili kurekebisha tatizo la mabadiliko ya majira ni lazima kutumia teknolojia mbadala mbali na fossil fuels. Mfano tunaweza kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya mto, nguvu za jua na upepo. Tunaweza kutengeneza mafuta ya magari kwa kutumia mafuta ya mazao (biofuel). Pia, tunaweza kupata gesi safi kutoka mbolea (biogas). Tunaweza kupanda miti ambayo huchukua carbon dioxide kutoka kwenye hewa wakati inakua. Carbon dioxide hiyo hutoka tena na kurudi hewani wakati miti hiyo inapounguzwa lakini kwa ujumla carbon dioxide haiongezeki (biomass).

Wachangiaji wakubwa wa shida hii ya mabadiliko ya majira ni nchi tajiri, kwa sababu wao wanatoa kiasi kikubwa sana cha carbon dioxide. Basi wana wajibu wa kupunguza kiasi cha carbon dioxide wanayozalisha na pia kusaidia nchi masikini kutumia technolojia mbadala.

Kwa hiyo basi, malengo ya msafara huu ni kama ifuatavyo:

- Kuelimisha wananchi kuhusu shida ya mabadiliko ya majira
- Kuonyesha watu na serikali ya Tanzania kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali wanaona umuhimu wa kushughulikia mabadiliko ya majira
- Kuujulisha ulimwengu kwamba watanzania wanaona umuhimu wa kushughulika mabadiliko ya majira

Pamoja na kipeperushi hiki, zimeambatanishwa barua mbili:

- barua kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kwa serikali ya Tanzania
- barua kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kwa Ubalozi wa Marekani

Barua hizi zimesainiwa na mashirika yafuatayo:

- Centre for Energy Environment Science & Technology (CEEST)
- Envirocare
- Joint Environment and Development Management Action (JEMA) – University of Dar es Salaam
- Journalists Environmental Association of Tanzania (JET)
- Legal and Human Rights Centre (LHRC)
- Tanzania Association of NGOs (TANGO)
- Tanzania Coalition for Sustainable Development (TCSD)
- Tanzania Traditional Energy Development and Environmental Organization (TaTEDO)
- Tanzania Youth Environment Network (TAYEN)
- Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)

Ratiba ya msafara jumamosi tarehe 8 Disemba ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Saa 2 asubuhi | Tunakutana pamoja ofisi ya Umma wa Wapanda Baisikeli Mabibo |
| Saa 2.30 asubuhi | Tunasafiri na baisikeli mpaka Ofisi ya Makamu wa Rais (karibu na posta ya zamani) |
| Saa 3 – saa 4 asubuhi | Tunakutana na wawakilishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Tunasoma barua kwa sauti na tunatoa maoni yetu kuhusu nini serikali ya Tanzania ifanye kuhusu shida ya mabadiliko ya majira. Tunapiga picha ya pamoja. |
| Saa 4 asubuhi | Tunasafiri na baisikeli mpaka Ubalozi wa Marekani |
| Saa 4.30 – saa 5.30 | Tunakutana na wawakilishi wa Ubalozi wa Marekani. Tunasoma barua kwa sauti na tunatoa maoni yetu kuhusu nini nchi za nje wafanye kuhusu shida ya mabadiliko ya majira. Tunapiga picha ya pamoja. |

Kwa taarifa zaidi:
Tanzania Coalition for Sustainable Development – Damas Nderumaki 0786 741964
Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA) – Elaine Baker 0754 568512 / Mejah Mbuya 0713 652642 / Dominata Rwechungura 0713 343477
www.globalclimatecampaign.org www.geocities.com/uwabadar

Kwa hiyo basi, malengo ya msafara huu ni kama ifuatavyo:

- Kuelimisha wananchi kuhusu shida ya mabadiliko ya majira
- Kuonyesha watu na serikali ya Tanzania kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali wanaona umuhimu wa kushughulikia mabadiliko ya majira
- Kuujulisha ulimwengu kwamba watanzania wanaona umuhimu wa kushughulika mabadiliko ya majira

Pamoja na kipeperushi hiki, zimeambatanishwa barua mbili:

- barua kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kwa serikali ya Tanzania
- barua kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kwa Ubalozi wa Marekani

Barua hizi zimesainiwa na mashirika yafuatayo:

- Centre for Energy Environment Science & Technology (CEEST)
- Envirocare
- Joint Environment and Development Management Action (JEMA) – University of Dar es Salaam
- Journalists Environmental Association of Tanzania (JET)
- Legal and Human Rights Centre (LHRC)
- Tanzania Association of NGOs (TANGO)
- Tanzania Coalition for Sustainable Development (TCSD)
- Tanzania Traditional Energy Development and Environmental Organization (TaTEDO)
- Tanzania Youth Environment Network (TAYEN)
- Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)

Ratiba ya msafara jumamosi tarehe 8 Disemba ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Saa 2 asubuhi | Tunakutana pamoja ofisi ya Umma wa Wapanda Baisikeli Mabibo |
| Saa 2.30 asubuhi | Tunasafiri na baisikeli mpaka Ofisi ya Makamu wa Rais (karibu na posta ya zamani) |
| Saa 3 – saa 4 asubuhi | Tunakutana na wawakilishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Tunasoma barua kwa sauti na tunatoa maoni yetu kuhusu nini serikali ya Tanzania ifanye kuhusu shida ya mabadiliko ya majira. Tunapiga picha ya pamoja. |
| Saa 4 asubuhi | Tunasafiri na baisikeli mpaka Ubalozi wa Marekani |
| Saa 4.30 – saa 5.30 | Tunakutana na wawakilishi wa Ubalozi wa Marekani. Tunasoma barua kwa sauti na tunatoa maoni yetu kuhusu nini nchi za nje wafanye kuhusu shida ya mabadiliko ya majira. Tunapiga picha ya pamoja. |

Kwa taarifa zaidi:
Tanzania Coalition for Sustainable Development – Damas Nderumaki 0786 741964
Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA) – Elaine Baker 0754 568512 / Mejah Mbuya 0713 652642 / Dominata Rwechungura 0713 343477
www.globalclimatecampaign.org www.geocities.com/uwabadar